



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA



3 Oktoba 2024

TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania, iliyokutana tarehe 2 Oktoba 2024 imeamua Riba ya Benki Kuu (CBR) kuendelea kuwa asilimia 6 kwa robo mwaka itakayoishia Disemba 2024. Uamuzi huu ulitokana na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kuwa chini ya lengo la nchi la asilimia 5. Kamati pia inatarajia uchumi kuendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha, sambamba na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani na hapa nchini.

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kukua sambamba na kuimarika kwa mazingira ya upatikanaji fedha. Kutokana na hali hii, Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia wanakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.2 na asilimia 2.6, mtawalia, mwaka 2024. Mwenendo huu unatarajiwa kuchagiza shughuli za uzalishaji hapa nchini. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua, ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ongezeko la ukwasi sambamba na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta na mbolea. Kutokana na hali hii, benki kuu katika nchi nyingi zinatarajiwa kupunguza au kutokubadili riba zao za sera ya fedha. Vilevile, benki kuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zinatarajiwa kufuata mwenendo huu wa kisera. Bei za bidhaa katika soko la dunia zimeendelea na zinatarajiwa kuendelea kuwa tulivu. Katika robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024, bei za mafuta ghafi zinatarajiwa kuwa kati ya dola za Marekani 72 hadi 82 kwa pipa, kutokana na ongezeko la uzalishaji. Hali hii inatarajiwa kupunguza ongezeko la mfumuko wa bei na mahitaji ya fedha za kigeni nchini kwa kuwa bidhaa za mafuta huchangia takriban asilimia 20 ya bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Kamati pia ilitathmini utekelezaji wa sera ya fedha katika robo mwaka inayoishia Septemba 2024, pamoja na mwenendo na mwelekeo wa uchumi hapa nchini. Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa sera ya fedha ulifanikiwa kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 5.

- i. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, uchumi ulikua kwa asilimia 5.6, huku shughuli za ujenzi, kilimo, fedha na bima, na usafirishaji zikichangia kwa kiwango kikubwa katika

ukuaji huu. Kwa mujibu wa viashiria vya awali, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.8 na asilimia 5.6 katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka 2024, mtawalia, na unatarajiwa kuendelea kukua katika viwango hivyo katika robo ya mwisho wa mwaka. Ukuaji huu utachangiwa na kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi hapa nchini na duniani. Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi nchini kunatokana na maboresho katika biashara na uwekezaji, ikiwemo yanayoendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Uzalishaji katika shughuli za kilimo unatarajiwa kuongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na matumizi ya pembejeo (mbolea na mbegu bora), viwatilifu na uwekezaji katika miradi ya umwagiliaji. Vilevile, shughuli za ujenzi na usafirishaji zinatarajiwa kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, ukichochewa na shughuli za usafirishaji, fedha na bima, na ujenzi.

- ii. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika jumuiya za kikanda. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3 na 3.1 mwezi Julai na Agosti 2024, mtawalia, na unatarajiwa kuwa asilimia 3.2 katika robo ya nne ya mwaka 2024. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu, ukichangiwa na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, upatikanaji wa chakula cha kutosha na umeme wa uhakika, pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na kibajeti. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi kufikia asilimia 5.1 kutokana na kushuka kwa bei bidhaa za chakula na zisizo za chakula. Hata hivyo, migogoro ya kisiasa Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati inaweza kusababisha kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi na kupelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.
- iii. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka kwa kasi ya kuridhisha ikiwa ni takriban asilimia 17.1 kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024, sawa na ukuaji uliofikiwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2024. Aidha, ubora wa rasilimali za benki uliendelea kuongezeka ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 3.9 mwezi Agosti 2024, kutoka asilimia 5.1 katika mwezi kama huo mwaka 2023. Mikopo kwa sekta binafsi inatarajiwa kuendelea kuongezeka, sambamba na kuimarika kwa uchumi wa dunia na wa hapa nchini.
- iv. Utekelezaji wa sera ya bajeti ulikuwa wa kuridhisha, ambapo mapato ya kodi yamevuka lengo, kufuatia kuimarika kwa usimamizi na kuongezeka ulipaji kodi kwa hiyari. Serikali imeendelea kupanga matumizi kulingana na mapato. Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 37,721.6, sawa na asilimia 46.9 ya Pato la Taifa (GDP), ambalo ni

chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi cha ukomo wa asilimia 60 kwa nchi za SADC. Wakati huohuo, uwiano wa deni kwa Pato la Taifa, kwa thamani halisi ya sasa (NPV) ulikuwa ni asilimia 36.4 mwaka 2023/24, chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi cha ukomo wa asilimia 50 kwa EAC.

- v. Sekta ya nje imeendelea kuimarika, sambamba na kupungua kwa athari za mitikisiko ya kiuchumi duniani. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (*current account deficit*) inakadiriwa kupungua hadi kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka ulioishia Septemba 2024 kutoka asilimia 4.4 ya Pato la Taifa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan utalii, dhahabu, tumbaku na korosho. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kusaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida unakadiriwa kuwa ziada ya dola za Marekani milioni 507, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 363.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, kutokana na kuongezeka kwa utalii na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa.
- vi. Upatikanaji wa fedha za kigeni uliimarika katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2024, sambamba na msimu wa shughuli za utalii na mauzo ya mazao ya kilimo na biashara nje ya nchi. Kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia pia kulichangia ongezeko la mapato ya fedha za kigeni nchini. Kutokana na mwenendo huu, kasi ya kuporomoka kwa thamani ya shilingi ilipungua hadi kufikia asilimia 10.1 kwa mwaka unaoishia Septemba 2024, kutoka asilimia 12.5 kwa mwaka ulioishia Juni 2024. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,413.6 mwishoni mwa Septemba 2024 kutoka dola za Marekani milioni 5,345.5 mnamo Juni 2024. Akiba hii inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa zaidi ya miezi 4, ambayo inaendana na lengo la nchi.

Upatikanaji wa fedha za kigeni unatarajiwa kuendelea kuimarika, kutokana na ongezeko la bei ya dhahabu kwenye soko la dunia, shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa asilia kama korosho, tumbaku, kahawa na pamba. Mauzo ya mazao ya chakula hususan mahindi na mchele kwenda nchi jirani, pia yanatarajiwa kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Wakati huohuo, kupungua kwa uagizaji wa mbolea na kupungua kwa bei za bidhaa za mafuta ya nishati kunatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni. Vilevile, matakwa ya kisheria kuhusu kunukuu na kufanya malipo ya ndani kwa shilingi ya Tanzania yanatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini na kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Aidha, Benki Kuu itaendelelea kuimarisha akiba ya fedha za

kigeni kupitia mpango wa ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani kwa kutumia Shilingi ya Tanzania.

EMMANUEL M. TUTUBA
GAVANA